SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la
# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 28, Aprili 2023

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

## BODI YA WAKURUGENZI KUTOKA LATRA WATEMBELEA MRADI WA SGR



Kaimu Mkurugenzi Mkuu TRC Bwana Senzige Kisenge akiwaonesha wajumbe wa bodi ya wakurugenzi LATRA baadhi ya picha za matukio ya ziara za viongozi mbalimbali katika mradi wa SGR ndani ya jengo la Stesheni jijini Dar es Salaam, Aprili 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania - TRC limepokea ugeni wa bodi ya wakurugenzi kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini - LATRA ambao wametembelea ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha kwanza Dar es Salaam - Morogoro kwenye jengo la stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam Aprili, 2023.

Mwenyekiti wa Bodi kutoka LATRA Prof. Ahmed Mohamed ameeleza kuwa Shirika la Reli limejipanga vizuri hasa katika masuala ya kiusalama kutokana na mifumo ya mawasiliano ambapo walitembelea katika chumba cha ishara na mawasiliano ndani ya jengo la stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam.

"Suala la uendeshaji wa reli linategemea sana usalama wa njia na vivuko pamoja na mapishano ya njia ya reli na barabara na kubwa zaidi kuweka uzio katika njia ya reli" alisema Prof. Ahmed.

**Inaendelea Uk. 2**

## BODI YA BOT YATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA RELI YA SGR Uk. 3



**Na Mwandishi wetu**

Bodi ya Wakurugenzi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BOT) wakiongozwa na Gavana wa Benki hiyo Bwana Emmanuel Tutuba watembelea ujenzi wa

**Inaendelea Uk.3**

# BODI YA WAKURUGENZI KUTOKA LATRA WATEMBELEA MRADI WA SGR



Meneja Msaidizi wa mrdi wa SGR Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi David Msusa (kulia) akiwaelezea wajumbe wa bodi ya wakurugenzi LATRA kuhusu mifumo ya kuongoza treni iliyopo ndani ya jengo la stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Aprili 2023.

**Inatoka Uk. 1**

Kaimu Mkurugenzi Mkuu kutoka TRC Bw. Senzige Kisenge alisema kuwa ugeni huo una manufaa makubwa katika uendeshaji wa mradi wa SGR kwa kupokea ushauri na maboresho ambayo yatauwezesha mradi kuwa bora.

Aidha Bw. Senzige alieleza kuwa TRC inaendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa wataalamu ambapo hadi sasa wataalamu 14 wapo nchini Korea Kusini na pia kuna mafunzo yanayotolewa ndani na mkandarasi ambapo wanafundishwa jinsi ya kuendesha mifumo mbalimbali.

"Mafunzo ni mengi ikiwemo ya umeme, mawasiliano na bado tutaendelea kutoa mafunzo kwa wataalamu wetu kwa awamu ili uendeshaji unapoanza tayari tuwe na wataalamu wa kutosha" alisema Bw. Senzige.

TRC inaendelea kusimamia mradi huo wa SGR kwa kuzingatia usalama wa watu pamoja na wanyama na kuendeleza mipango mbalimbali ya kutoa uelewa kwa wananchi kabla na baada ya mradi kuanza uendeshaji.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu TRC Bwana Senzige Kisenge akifafanua jambo kwa bodi ya wakurugenzi LATRA walipofanya ziara kutembelea mradi wa SGR katika jengo la stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Aprili 2023.

# BODI YA BOT YATEMBELEA MRADI WA UJENZI WA RELI YA SGR



Wajumbe wa Bodi ya Benki Kuu ya Tanzania wakipata maelezo kutoka kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu TRC Bwana Senzige Kisenge (wa tano kushoto) kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR katika jengo la stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Aprili 2023.

Inatoka Uk. 1

reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kipande cha kwanza kutoka Dar es Salaam - Morogoro katika Stesheni ya Dar ss Salaam, Aprili 2023.

Lengo la ziara hiyo ni kukagua na kujionea uwekezaji uliofanywa na Serikali katika jitihada za kuendeleza na kukuza sekta ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia ukuaji wa uchumi miongoni mwa sekta hizo ni Reli na Bandari.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Ndugu Emmanuel Tutuba amesema kuwa BOT itahakikisha inabuni mbinu na kuunda mikakati ambayo itawezesha nchi kupata fedha za kigeni kupitia sekta za kiuchimu ambazo Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa katika kuzijenga na kuziendeleza ikiwemo mradi wa ujenzi wa SGR.

"Kwa mujibu wa Sheria BOT tunawajibu na dhamana ya kusimamia masuala mbalimbali ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuangalia mapato hasa namna tukavyoweza kupata dola za kimarekani au fedha za kigeni, tumeona namna ambavyo serikali imewekeza kwenye SGR, eneo la Kwala kuna maeneo ambayo reli hii itafika kwenye viwanda na bandari kavu eneo la TPA ambalo litaunganishwa na reli na kuchukua mzigo kwenda maeneo mbalimbali na nchi za nje, hii italeta fedha nyingi za kigeni na kusaidia nchi kukua kiuchumi" Amesema Bwana Tutuba.

Aidha, Bwana Tutuba ameongeza kuwa BOT imeshauriana na TRC, TPA pamoja na EPZA kuunda mipango na mikakati itakayowezesha uchumi wa wananchi, mashirika, makampuni pamoja na mapato ya Serikali na nchi kwa ujumla kuunganishwa kwa pamoja ili kuboresha biashara ya Kimataifa kwa kukuza mauzo ya nje na kupata fedha za kigeni.

"Uwekezaji huu wa SGR ni kweli umelenga kukuza uchumi, tulikuwa tunashauriana namna ambavyo uchumi wa mtu mmoja moja, uchumi wa makampuni, uchumi upande wa Serikali yaani mapato na nchi kwa ujumla utakavyoweza kuunganishwa ili tukuze mauzo ya kwenda nje, tukiongeza mauzo nje tunapata fedha nyingi za kigeni, kwa hiyo kuna mpango ambao tunaendelea kuangalia kama Benki Kuu kwa kushirikiana na serikali unaitwa mkakati wa Kukuza mauzo nje (import substitution initiative) na kuangalia mbadala wa vile vitu tunavyoingiza ndani kutoka nje viweze kuzalishwa ndani" Amesema Bwana Tutuba.

# WADAU SEKTA BINAFSI WAKUTANA NA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI

**Na Mwandishi wetu**

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa ameshiriki katika ufunguzi wa kongamano kati ya Sekta ya Uchukuzi na wadau wa sekta Binafsi (Ministerial Public Private Sector Dialogue – MPPD) lililofanyika katika ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNICC), Aprili 2023.

Kongamano limekusudiwa kujadili shughuli zilizofanyika ndani ya kipindi cha mwaka mmoja katika sekta ya uchukuzi, changamoto zinazoikumba sekta ya uchukuzi, mafanikio ndani ya mwaka mzima, pia kujadili sera na mikakati ya nchi inayolenga kukuza sekta ya uchukuzi nchini ili kuleta mafanikio.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa amezitaka Mamlaka za Serikali kushirikiana na wafanya biashara kuhakikisha changamoto zinazowakabili zinatatuliwa haraka ili kurahisisha mazingira ya ufanyaji biashara Tanzania.

“Nipende kusema kuwa sekta binafsi ni wadau wakubwa sana wa Serikali, pengine kuna kanuni au taratibu ambazo zinawakwaza, sisi tuko maofisini nyinyi mnafahamu kuliko sisi, kupitia mikutano hii tunaamini tunaweza kujua na kuzifanyia kazi“ amesema Mbarawa.

Aidha, Mheshimiwa Mbarawa ameongeza kuwa Serikali kupitia Wizara ya ujenzi na uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) imelenga kujadiliana na sekta binafsi kupitia mikutano na makongamano mbalimbali ili kuzifahamu fursa, maboresho ya Sera, Sheria , kanuni na miongozo mbalimbali ili kujenga mzingira mazuri ya biashara .

“Ndugu washiriki Mheshimiwa Raisi Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuagiza kwamba Wizara ikutane na sekta binafsi katika maeneo yetu ili kupokea maoni, changamoto na maboresho ya sera, Sheria na miongozo mbalimbali kwasababu bila kuwa na Sheria nzuri na kanuni nzuri zinazoendana na wakati hatuwezi kufanya biashara na kushindana na wengine” amesema Mbarawa.

Naye Mwenyekiti wa Sekta Binafsi nchini Bi. Angelina Ngalula amesema sekta ya uchukuzi inasaidia kupunguza gharama za bidhaa zinazozalishwa nchini haswa katika sekta ya kilimo hivyo kuitaka Serikali iipe sekta ya uchukuzi kipaumbele kwa kuendeleza miundombinu ikiwemo reli na barabara.

"ukuaji wa sekta ya uchukuzi, itasaidia katika kupunguza gharama za bidhaa zinazozalishwa nchini hasa za kilimo, utakuta bidhaa kutoka China inauzwa gharama kuliko inayozalishwa hapa nchini, hii ni kutokana na gharama kubwa katika usafirishaji “ amesema Bi. Ngalula.

“Nchi yetu ni ya kimkakati, ina fursa nyingi, katika sekta hii tutambue sisi ni wanachama wa SADC, kwahiyo tunapojadili Sera, mikakati na mambo madhubuti ya nchi, lazima tutunge Sera zinazoendana na ushindani wa soko, zikiwa Sera tofauti sisi ndio tutakaopoteza zaidi” alisema Bi. Angelina.



Baadhi ya wadau wa Sekta binafsi waliohudhuria kongamano maalumu la wadau wa sekta binafsi nchini katika ukumbi wa kimataifa wa mikutano wa Mwalimu Julius Nyerere jijini nDar es Salaa, April 2023.

# MAENEO YAENDELEA KUTWALIWA MKOA WA PWANI KUPISHA MRADI WA SGR



Afisa Ardhi kutoka TRV Beatrice Luhimbo (wa pili kushoto) akimsainisha Bi. Maua Budi (aliyesimama) katika zoezi la ulipaji fidia lililofanyika katika ofisi ta Serikali ya kijiji cha Kwala mkoani Pwani Aprili, 2023.

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania – TRC linaendelea la zoezi la ulipaji wa fidia kwa wananchi waliotwaliwa ardhi zao kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa – SGR kipande cha kwanza Dar es Salaam – Morogoro katika mtaa wa Kwala, Makutupora pamoja na Kikongo wilayani Kibaha mkoa wa Pwani hivi karibuni Aprili, 2023.

Afisa Ardhi kutoka TRC Bi. Beatrice Luhimbo alisema kuwa zoezi lililofanyika ni kutokana na maeneo yaliyoongezwa na mkandarasi kwaajili ya ujenzi wa njia ya juu ya reli ya kisasa pamoja na eneo la kuweka udongo usiohitajika katika ujenzi.

“Mkandarasi anaongeza eneo pale anapokuwa na uhitaji kwasababu SGR ni mradi wa kusanifu na kujenga, ikitokea hivyo mwananchi anafanyiwa uthamini wa eneo na baadae anapatiwa stahiki zake” alisema Bi. Beatrice.

Mtendaji kutoka katika Kata ya Kwala iliyopo wilaya ya Kibaha Bw. Burton Mwaselela ameeleza kuwa wananchi wasisite kuendelea kutoa maeneo pindi yatakapohitajika ili kupisha ujenzi huo wa reli yenye kiwango cha kimataifa kwani reli hiyo italeta tija na chachu ya maendeleo kwatika maeneo itakapopita.

“Serikali inaweka juhudi kubwa kuhakikisha wananchi wanafaidi matunda ya kodi zao kupitia miradi mikubwa ukiwemo mradi huu wa SGR hivyo tuendelee kushirikiana na viongozi waliopo madarakani ili kuwapa nguvu ya kuinua taifa letu” alisema Bw. Mwaselela.

Mwananchi kutoka kijiji cha Makutupora Bw. Saidi Garama alisema kuwa mradi wa SGR utaleta mwangaza katika kukuza pato la taifa pamoja na wananchi, pia kwa kizazi cha baadae kwakuwa ni reli ambayo ina uwezo wa kudumu kwa miaka mingi.

Shirika la Reli Tanzania linaendelea kushirikiana na wananchi kuhakikisha wanapata stahiki zao kwa kufuata utaratibu mzuri uliowekwa na Serikali na kusaidia kutatua changamoto yoyote inayojitokeza kwa wananchi waliotwaliwa maeneo yao.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Dkt. Ally Possi (aliyevaa shati jekundu) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Kampuni ya Sung Shin Rolling Stock ya nchini Korea Kusini mara baada ya kukagua karakana ya utengenezaji wa vichwa na mabehewa ya SGR, Aprili 2023.



Kaimu Mkurugenzi Udhibiti wa Usafiri wa Reli - LATRA Mhandisi Hanya Mbawala akimuelezea jambo Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi LATRA katika eneo la Karakana na kituo cha treni za mizigo Kwala mkoani Pwani, Aprili 2023.



Mtaalamu wa Masuala ya kijamii kutoka TRC Suzan Simkwayi akiwaelezea wananchi wa kijiji cha Tambuka reli kuhusu utaratibu wa zoezi la utwaaji ardhi ili kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kipande cha Makutupora - Tabora, Aprili 2023.



Mhandisi wa Mradi kutoka TRC Juma Lugema akizungumza na wananchi wa kijiji cha Karangasi katika kikao cha uhamasishaji kwaajili ya zoezi la utwaaji ardhi ili kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kipande cha Makutupora - Tabora, Aprili 2023.



Mkuu wa Wilaya ya Uyui Ndugu Zakaria Mwansasu akizungumza na wananchi wa kijiji cha Igalula wakati wa kikao cha uhamasishaji wa utwaaji ardhi kwaajili ya kupisha ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Makutupora - Tabora, Aprili 2023



Wananchi wa kijiji cha Malongwe wilaya ya Uyui wakiwa katika kikao cha uhamasishaji wa utwaaji ardhi kwaajili ya kupisha ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Makutupora - Tabora, Aprili 2023

# DC UYUI AWATAKA WANANCHI KUTOA USHIRIKIANO KATIKA ZOEZI LA UTWAAJI ARDHI

**Na Mwandishi Wetu**

Mkuu wa Wilaya ya Uyui Ndugu Zakaria Mwansasu amewataka wananchi wa kijiji cha Malongwe kutoa ushirikiano kwa timu kutoka Shirika la Reli Tanzania - TRC katika zoezi la utwaaji ardhi linaloendelea mkoani Tabora, Aprili 2023.

Ndugu Mwansasu alizungumza na wananchi katika mkutano wa uhamasishaji uliofanyika kwaajili ya maandalizi ya utwaaji ardhi kupitia uhamishaji wa makaburi yaliyopitiwa na mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kipande cha tatu Makutupora – Tabora kwa lengo la kumpatia eneo mkandarasi aweze kuendelea na ujenzi.

"Serikali inajenga miundombinu, ni ya kwetu na inatumia fedha nyingi, hivyo nawaomba mtoe ushirikiano kwa timu hii na asiwepo mtu yeyote atakayekwamisha zoezi" alisema Mwansasu

Mhandisi Rajab Mahaja kutoka TRC alifafanua utaratibu wa uhamishaji makaburi ambapo makaburi yaliyopitiwa na mradi yataainishwa na kuhamishwa kwa kuzingatia taratibu za afya kupitia wataalamu wa afya wa Wilaya na kuhamishiwa katika maeneo rasmi kwa kufuata taratibu za imani ya Dini husika.

"Maeneo yatakayochukuliwa kwaajili ya ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa yatahusisha maeneo kwaajili ya kuchukua kifusi, maeneo ya kutupa kifusi kisichofaa kwa ujenzi na maeneo ya ujenzi wa miundombinu ya reli" aliongeza Mhandisi Mahaja.

Mtaalamu wa Afya kutoka Wilaya ya Uyui Bi. Mary Kayombo aliwasisitiza wananchi kujitokeza siku ya zoezi la uhamishaji ili kuhakikisha makaburi yanahamishiwa katika maeneo rasmi yaliyopangwa na Serikali ya kijiji. Vilevile aliwasihi wananchi kuacha kuzika katika maeneo ya makazi ili kuepusha uhamishaji wa makaburi katika maeneo ya makazi pindi miradi ya maendeleo inapotaka kutekelezwa.

Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa Dar es Salaam kuelekea Mwanza na Kigoma. Miongoni mwa shughuli za awali za utekelezaji wa mradi ni utwaaji wa ardhi ili kukabidhi maeneo kwa mkandarasi aweze kuendelea na ujenzi. Mradi wa SGR unatekelezwa kwa mtindo wa sanifu jenga, hivyo zoezi la utwaaji ardhi ni endelevu kulingana na mahitaji ya mkandarasi.



Timu kutoka Shirika la Reli Tanzania wakiwa katika kikao na Mkuu wa Wilaya ya Uyui Ndugu Zakaria Mwansasu kwaajili ya maandalizi ya zoezi la utwaaji ardhi kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR kipande cha Makutupora - Tabora, Aprili 2023.



Mkuu wa Wilaya ya Uyui Ndugu Zakaria Mwansasu akizungumza na wananchi wa kijiji cha Malongwe wakati wa kikao cha uhamasishaji wa utwaaji ardhi kwaajili ya kupisha ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Makutupora - Tabora, Aprili 2023

# MAENDELEO YA MRADI WA SGR MWANZA - ISAKA



Kazi ya kuweka reli ya kiwango cha kimataifa - SGR juu ya tuta ikiendelea mkoani Simiyu katika mradi wa SGR kipande cha Mwanza - Isaka-hivi karibuni Aprili 2023.



Ujenzi wa jengo la stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Seke mkoani Simiyu ikiendelea katika mradi wa SGR kipande cha Mwanza - Isaka, Aprili 2023.



Ujenzi wa jengo la stesheni ya reli ya kiwango cha kimataifa - SGR Bukwimba mkoani Mwanza ikiendelea katika mradi wa SGR kipande cha Mwanza - Isaka, Aprili 2023.



Kazi ya ujenzi wa daraja refu la reli ya kiwango cha kimataifa linalokatiza katikati ya jiji la Mwanza ikiendelea katika mradi wa SGR kipande cha Mwanza - Isaka, Aprili 2023.



Kazi ya ujenzi wa daraja la reli ya kiwango cha kimataifa ikiendelea wakati wa usiku katika mradi wa SGR kipande cha Mwanza - Isaka, Aprili 2023..

# KIJUE CHUO CHA TEKNOLOJIA YA RELI TANZANIA (TIRTEC)g9




**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania lilianzishwa wakati wa ukoloni, ili twende sambamba tuanze kuangazia mwaka 1948 lilipoanzishwa Shirika la Reli na Bandari za Afrika Mashariki (EAR&H). Shirika la reli na bandari za Afrika ya Mashariki liliundwa mnamo mwaka 1948 sambamba na Jumuiya ya Afrika Mashariki na lilikuwa Shirika la umma lililosimamia reli na bandari za Kenya, Uganda na Tanganyika na baadaye Tanzania. Shirika la Reli lilikuwa na majukumu mbalimbali, moja ya majukumu ni kuandaa wataalamu kwaajili ya kusimamia na kuendesha shughuli za lililokuwa Shirika la Reli na Banadari la Afrika Mashariki.

Mwaka 1947 Shirika lilianzisha Chuo cha Teknolojia ya Reli Tabora (TIRTEC) wakati huo kilikuwa kikitambulika kama Chuo cha Mafunzo ya Reli (RATCO) likiwa tawi la Shule ya Mafunzo ya Reli (Railway Training School) iliyokuwa na makao makuu yake Nairobi nchini Kenya ili kujipatia wafanyakazi wenye weledi kwenye technolojia ya reli. Chuo kilianzishwa mara baada ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

RATCO ilikuwa mojawapo ya Idara za Shirika la Reli na Bandari za Afrika Mashariki (EAR&H) ambayo madhumuni yake yalikuwa kuunda upanuzi wa shule kuu ya Nairobi kwaajili ya kuendesha mafunzo ya kada za chini na za kati za Idara ya Usafiri wa Reli ambayo haikuweza kushughulikiwa katika Shule ya Nairobi. Kada hizo ni pamoja na Makarani wa Vituo, Walinzi wa Treni (Train Guards), Wakaguzi wa Tiketi, Wasimamizi wa Yard na Wasaidizi wa Vituo. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Chuo cha Teknolojia ya Reli ni kutoa mafunzo ya reli na kuandaa wataalamu katika nyanja mbalimbali kwaajili ya kuendesha shughuli za lililokuwa Shirika la Reli na Bandari Afrika Mashariki.

Kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, Chuo kilijitegemea na kuendelea kutoa mafunzo kwa madaraja ya III, II na I kwa kozi zote. Hii ni pamoja na kozi za Mafundi wa kutengeneza vichwa vya treni, Mafundi wa njia ya reli, Mafundi wa Ishara na Mawasiliano, pia Wakaguzi wa mabehewa (CXR).

Kutokana na kupanuka kwa mafunzo, mwaka 1979 Novemba, Chuo kilifungua tawi lake kwenye Karakana ya Reli Morogoro kwa kozi za mafundi wa kutengeneza vichwa vya treni. Baadaye mwaka 1994, kozi ya madereva wa kuendesha treni pia ilihamishiwa Morogoro. Sababu kuu ya kuhamishia kozi hizi Morogoro ni kurahisisha mafunzo ya

# KIJUE CHUO CHA TEKNOLOJIA YA RELI TANZANIA (TIRTEC)

Inatoka Uk. 10

vitendo kwa maana ya nadharia darasani na vitendo kwenye karakana.

Mwaka 1989, kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani, majengo ya Hostel na madarasa kwa ajili ya Idara ya Ishara na Mawasiliano yaliongezwa katika kampasi kuu ya Tabora.

Chuo kina kampasi mbili; kampasi kuu ya Tabora na kampasi ya Morogoro. Chuo kimesajiliwa kwa jina la 'TANZANIA INSTITUTE OF RAILWAY TECHNOLOGY' yaani Chuo cha Teknologia ya Reli Tanzania. Chuo kimesajiliwa na NACTVET kama chuo cha kufundisha elimu ya ufundi kwa sheria ya NACTE namba 9 ya mwaka 1997 inayohusu vyuo vya elimu ya ufundi.

Jina la chuo lilibadilika kutoka Chuo cha Mafunzo ya Reli (RATCO) na kuwa Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania (TIRTEC) baada ya kusajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) tarehe 12 Septemba, 2008.




Baadhi ya Wanafunzi wanaosome ufundi wa matengenezo ya vichwa na injini za vichwa vya treni katika kampasi ya Morogoro.

Kampasi ya Tabora imesajiliwa na NACTE kwa namba ya usajili REG/EOS/012 mnamo tarehe 12/09/2008 na kampasi ya Morogoro imesajiliwa kwa namba REG/SAT/044 mnamo tarehe 30/07/2019.

Chuo kimepata ithibati kutoka NACTVET ya kufundisha kozi za Stashahada ya Usafirishaji kwenye njia ya Reli (Ordinary Diploma in Rail Transportation - NTA Level 4 - 6), Astashahada ya Teknolojia ya Ukaguzi, Ukarabati na Matengenezo ya Mabehewa (Technician Certificate in Carriage and Wagon Technology - NTA 5), Astashahada ya Awali ya Teknolojia ya Ukaguzi, Ukarabati na Matengenezo ya Miundombinu ya Reli (NTA Level 4.

Kozi zote za Chuo ziko kwa vijana wa kitanzania na nje ya nchi wenye sifa za kufaulu vema mitihani ya kidato cha IV au VI au kozi za VETA (NTA Level III) zinazoendana na kozi anayotaka kusoma hapo chuoni. Kwa kutumia rasilimali zilizopo, Chuo kina uwezo wa kudahili wanafunzi 400 kwa Kampasi ya Tabora na wanafunzi 260 kwa Kampasi ya Morogoro.

Chuo kina mawasiliano na vyuo vingine vya nje vinavyofundisha kozi zinazowiana na chuo ili kubadilishana ujuzi na uzoefu na hatimaye kuboresha mafunzo. Baadhi ya vyuo hivyo ni Railway Meles Zenawi Memorial TVET, Ethiopia Railway Academy (Nchini Ethiopia), Mpika Training College (TAZARA – Zambia), na vyuo vingine vya Korea Kusini na China.

Chuo cha Reli (TIRTEC) kinategemea kuanzisha kozi ambazo zitazalisha wataalamu wa kusimamia biashara ya usafirishaji kwa njia ya reli ya kisasa. Mitaala ya kozi hizi maandalizi yake yapo mbioni kuanza ili kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia katika Sekta ya Reli.

Shirika la Reli Tanzania kupitia mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR Tabora – Isaka linatarajia kufanya maboresho makubwa katika chuo cha reli ili kukiongezea uwezo wa kudahili wanafunzi wengi hadi ngazi ya Shahada katika taaluma mbalimbali za reli hususani upande wa uendeshaji wa reli ya kisasa – SGR.



Baadhi ya wahitimu wa kozi mbalimbali katika chuo cha reli Tabora wakiwa katika picha na baadhi ya viongozi wa mkoa wa Tabora, Shirika na Chuo.



**BODI YA WAHARIRI**
**MHARIRI MKUU | Jamila Mbarouk, MHARIRI MSAIDIZI/MSANIFU | Sami Omary**
**HABARI | Hemed Mohamed, Mariam Katunge MAKALA | Aziza Charles, Amina Juma, Athumani Iddy**
**PICHA | Musa Kadiko, Hassan Mbonde, Augustino Bulegea**